## Semina Agape

# UKUAJI KIROHO

## Safari
**kutoka Misri kwenda Kanaani**
**Kutoka hali ya kibinadamu**
**Kwenda hali ya kimungu**

**Kitabu hiki kimetayarishwa**
**na**
**Imetungwa na Sr. Cordula MAFOI**

**Agape Publications**
**P.O.Box 76021 Dar-es-Salaam**
**Simu : 022 2420465**
**e-mail agape@intafrica.com**

# Utangulizi

Hali yetu kiroho inahitaji kukua. Hali hiyo ya kiroho ndio Ufalme wa Mungu ndani mwetu, ambao machoni pa watu ni kitu kidogo sana kisichoonekana kwa urahisi. Kwa wengi huonekana tu baada ya kumaliza shughuli za kawaida za kidunia. Kwa macho ya kawaida Ufalme wa Mungu ni mdogo sana, na watu hawana muda kwa mambo madogo. Ufalme huo kwa mtazamo mwingine ni kitu kinachokua, na uwezo wake wa kukua ni mkubwa sana, nao hukua na kuwa mkubwa kuliko matarajio ya watu. Nidyo maana Yesu alisema :
"Utawala wa Mbinguni umefanana na mbegu ya haradali … yenyewe ni ndogo kuliko mbegu zote, lakini ikioteshwa huwa kubwa kuliko mimea yote, hata ikawa mti" Mt. 13:31-32.
Tuangalie kwa pamoja kukua kwa huu utawala wa Mungu ndani mwetu, tukiufananisha pia na safari, hasa safari maalumu waliosafiri Waisraeli kutoka Misri Utumwani kwenda Kanaani nchi ya Ahadi. Tutaona Utumwa wa kiroho, jangwa la kiroho na nchi tuliyoahidiwa kiroho.
Jinsi safari ya Waisraeli ilivyokuwa ya ajabu na ngumu, ndivyo ilivyo safari ya kiroho. Njiani vizuizi na vipingamizi ni vingi kama ilivyokuwa kwa Waisraeli kule jangwani. Watakaoshikamana na Bwana mpaka mwisho ndio watakaoingia katika nchi ya Ahadi ambayo ni muungamo kamili na Mungu.

# Siku ya 1
# Waisraeli Utumwani Misri.

Soma Kut.1:1-2:25.

## **Maisha kabla ya kumtambua Mungu** (Early Purgative)

Jinsi ambavyo wazao wote wa Yakobo walivyokulia Misri, yaani wote walikwenda kuishi Misri bila kubaki hata mmoja, ndiyvo ilivyo kwetu sisi sote kiroho. Sote tumetindikiwa Neema ya Mungu, sote tunahitaji kukombolewa. Kwa maneno hayo ninataka kusema : "sisi sote tumezaliwa utumwani Misri, sote tumejeruhiwa kwa kutumikishwa kwingi".

Kabla ya kuendelea inafaa tujiulize : Utumwa wetu wa kiroho ni wa namna gani ? Tukumbuke kuwa mtu aliumbwa kwa ajili ya Mungu tu, hivyo kila mwanadamu anayo hamu ya kuunganishwa na Mungu Muumba wake. Mtu atake asitake, moyo wake hautulii, unamtafuta Muumba wake usiku na mchana bila hata yeye kujua. Katika kutafuta huko, watu wengi, mamilioni ya watu, wanapotea njia. Wanamtafuta Mungu kweli lakini asikopatikana. Wakati huo huo hawajui hata wanachotafuta ! Hawatulii, hawapati raha, wanainuka tena na tena kutafuta. Wanamtafuta Mungu lakini hawajui kuwa ni Mungu wanamtafuta. Ninasema hivyo kwa sababu watu wote duniani wana mwelekeo wa kutafuta : Heri, Uzima, Utamu, Raha … yote haya na mengine mengi ndio watu wanayotafuta. Ukweli ni kwamba chochote kizuri kinachofurahisha, asili yake ni Mungu.
Mungu ndiye utamu wenyewe, ndiye heri yenyewe, ndiye asili ya chochote kilicho kizuri. Kwa maana hiyo ni kwamba, kwa kuyatafuta hayo, ni Mungu wanamtafuta bila wao kujua ! Mbaya zaidi ni kwamba, kumtafuta bila kumjua na bila kumtaja hakutoshelezi mtu ! Hakutoshelizi kwa sababu waweza kupita karibu naye sana, ukampita na kuendelea mbele ukimtafuta kwa sababu hata ukimwona humjui ! Muda wote maisha yote itakuwa ni kutafuta mbugani bila mafanikio mpaka yeye mwenyewe awe na huruma na kujitambulisha.

Tuangalie ukweli wa maisha katika kumtafuta Mungu asikopatikana na mtu kutotulia. Tuchukue mfanya biashara. Alianza chini sana hata baiskeli hakuwa nayo akatamani kuipata ili kazi yake iende haraka. Akafanikiwa kuipata. Akaona pikipiki inaharakisha zaidi, akajitahidi kujinyima starehe fulani fulani akafaulu kununua pikipiki. Akaendelea hivyo akanunua gari, akaendelea akanunua magari makubwa zaidi ya kumi ya kupeleka abiria mikoani, akaendelea na sasa anatamani kununua ndege awapeleke watu kwenye mabara mengine ! Nasema wazi kuwa hata akifaulu kwa hili bado hatatosheka. Kwenye moyo wake, yaani moyoni mwake ndani kabisa atajisikia mtupu ! Aweza kujitokeza mbele za watu kama tajiri, lakini ndani mwake anajisikia maskini na mtupu ! Kwa nini ? Bada hajapata anachotafuta.

Siyo kwa masuala ya biashara na mali tu, bali ni kwa kila kitu ambacho mtu anatumia nguvu zake kukipata. Siyo vitu tu bali hata hali. Mtu anatamani kupata sifa, kuheshimiwa, kuwa mzuri, kupendwa, afya nzuri, yote hayo na mengine mengi ni Mungu wanamtafuta bila wao kujua. Watu wanakwenda kwa waganga na kushiriki katika ushirikina; hapo ni uhai wanautetea bila kujua uhai wa kudumu hupatikana kwa Mungu tu ! Wengine wanaenda hata kinyume na maumbile kwa kufanya matendo ya uasherati wa aina aina, hamu yao ni kupata raha, raha ya pekee zaidi, wasijue raha zote za kila namna hupatikana mbinguni kwa Mungu tu, na hapa kwa kufanya hivyo ni kama kuiba au kudokoa kile ambacho kingekuwa chao kwa milele yote ! Wanamtafuta Mungu bila kujua na bila kumtaja.

Wanafanana na mtoto Happy aliyepotea sokoni akawa analia sana hata watu wakamwonea huruma.

Wakamuliza : Unaitwa nani ?
Mtoto anajibu akilia : Ninaitwa Happy !
Wanamwuliza tena : Baba yako anaitwa nani ?
Mtoto anajibu : Anaitwa baba Happy !
Wanaendelea kumwuliza : Mama yako anaitwa nani ?
Mtoto anajibu tena : Anaitwa mama Happy !
Wanajaribu kuuliza swali lingine : Kwenu ni wapi ?
Anajibu : Kwetu ni nyumbani …

Tumeumbwa kwa sura na mfano wa Mungu (Mwa.1:26). Hapa mtu anasahau kuwa ameumbwa akabaki na neno 'Sura na Mfano', na hivyo kutaka kujitwalia ule urithi wa kimungu kabla ya kumtambua Mwumba. Tunafanana na mtoto aliyekulia mbali na nyumbani, mbali na wazazi akasikia kuwa wazazi wake ni wazuri na ni matajiri, naye akasafiri akafika kwa wazazi wake, akawakuta wafanyakazi, bila kuuliza habari za wazazi, wamwonyeshe urithi wake aliotengewa, akaanza kutamalaki ! Baba kwake si kitu, kitu kwake ni urithi ! Baba akipata habari atajisikiaje ? Atafanya nini ? Pengine wafanyakazi kwa vile hawajui mipango yote ya Baba, walipitiwa wakamwonyesha sehemu ambayo ilikuwa ni ya ndugu yake, na hapo kutatokea tena fujo !

Huu ndio utumwa wetu wa Misri. Akili zetu, tamaa zetu, mivuto yetu, vyote vinatutumikisha ! Hatumwendei Baba na kupata maana na namna ya kutumia vyote hivi, tunajiamulia cha kufanya. Tumwombe Mungu atuhurumie na hivyo atufungue macho !

## Masomo ya Tafakari

Semina hii lengo hasa ni kumsaidia mtu binafsi aweze kujigundua yupo wapi katika safari yake ya kiroho. Hivyo badala ya mjadala kutakuwa na masomo ya kutafakari. Mtu atafanya mjadala na Mungu na nafsi yake, akisaidia na masomo katika biblia.

| | |
|---|---|
| 1 Fal.19:1-13 | Unafanya nini hapa ? |
| Ufu.3:20 | Nasimama mlangoni nabisha |
| Mk.10:46-52 | Bartimayo |
| Mt. 11:28-30 | Njoni kwangu ninyi nyote mnaosumbuka. |
| Lk;10:38-42 | Maria na Martha |
| 1 Sam.3:1-11 | Nena Bwana mtumishi wako anasikia |
| Mik. 6:6-8 | Kuishi kwa unyenyekevu na Mungu wako. |
| Yer. 29:1-14 | Ndiyo, utakaponitafuta kwa moyo wakao wote, utanipata |

******************************

# Siku ya 2
# Mungu anamwita Mungu awatoe Waisraeli utumwani Misri

Soma Kut.3:1-10,12:21-15:4

## Neema za Mungu (Middle purgative)

Sisi sote tumezaliwa Misri, yaani sote tumezaliwa katika hali inayotuvuta katika dhambi, inayotuvuta kujisaidia au kujikomboa wenyewe bila Mungu. Mungu kwa huruma yake anaona udhaifu wetu, anaona wazi kuwa bila msaada wake hatutaweza kamwe kumgundua. Kwa huruma yake akaamua kutupelekea misaada mbali mbali, ili mwenye kuona aone, mwenye kushtuka ashtuke na mwenye masikio asikie. Misaada hii hutujia kama umeme toka mbinguni, bila mtu kutazamia. Hii inaitwa 'Neema za misaada'. Neema hizi humfikia kila mtu na popote. Neema hizi si kwa wakristo tu au watu fulani tu, ni kwa kila mtu, itamtegemea mtu kama yupo tayari au sivyo ! Hii kwa hakika ni zawadi ya Mungu kwetu. Zawadi haiombwi wala haishurutishwi ! Waweza kuipokea na kuitumia vizuri au kuikataa na kuitupa.

Mungu kwa hekima yake kuu amefanya hivi ili kuheshimu maumbile yetu ambayo ndiyo zawadi ya kwanza aliyotukirimia : 'Sura na mfano wake !' Hii hadhi yetu ya Kimungu inamfanya Mungu atupatie uhuru kama wake, tuamue wenyewe kuungana naye au la ! Ndiyo maana ataendelea kutoa neema bila kushurutishwa.

Tukiwaangalia Waisraeli, tunaona walivyotumikishwa, na Mungu akawaonea huruma akamtuma Musa kama neema ya msaada kwao, ili awaoongoze watoke utumwani. Kabla ya Musa kutumwa, tunaona wazi kuwa waliteseka sana. Hata kwetu siku hizi, ili mtu apate neema za msaada ni lazima ajitambue kuwa anateseka. Kwa wengine mateso hayo yaweza kuwa makali sana na ya muda mrefu, kwa wengine

mateso yaweza yasichukue muda mrefu. Wakati maalumu unapofika, Mungu anapeleka msaada.

## Kuvuka Bahari ya Shamu

Utumwa wa Waisraeli uliendelea hadi walipovuka ile bahari ya Shamu. Mara baada ya kuvuka ndipo walipoweza kuona wazi kuwa Mungu alikuwa pamoja nao **akiwapigania.** Ndipo walipoimba kwa shangwe na kumhimidi Mungu wa Ibrahimu, Isaka na Yakobo. Tangu pale ng'ambo ya bahari walianza maisha mapya kabisa.

Kwetu sisi kitu chochote chaweza kutuvusha :
Yawezekana kuwa kuokoka katika ajali ya gari au meli, au kifo cha mtu wa karibu, na ugonjwa wa hatari, au matukio katika maisha kama vile sherehe za Ekaristi, Upadrisho, Ndoa … Mungu aweza kutumia chochote kadiri ya mtu huyo.

Tukio hilo linapomfika mtu, linampiga kama mwanga mkali, ni kama kutazama jua kwa macho. Mwanga unakuwa mkali kiasi cha kutoona tena kadiri ya mtazamo wa kawaida, mtazamo wa awali. Yote yanageuka, njia na mwelekeo vinabadilika. Anajazwa na FURAHA isiyoelezeka, hata akijitahidi kueleza namna gani, hakuna atakayemwelea isipokuwa tu wale waliokwisha pita hatua hiyo. Ndiyo maana wengine wakifika hapo wanasema : 'Nimeokoka'. Kuanzia pale, mtu akiendelea kuwa msikivu kwa Mungu, maisha hubadilika kabisa, huwa mtu mpya. Tukio hilo au neema hizo ni Mungu mwenyewe amejitokeza kwa mwanga mkubwa. Mtu aliyeona utukufu wa Mungu, anapojiangalia anajiona alivyopungukiwa utukufu huo. Ni kama Nabii Isaya alivyouona utukufu wa Mungu alilia :

"Ole wangu! Kwa maana nimepotea; kwa sababu mimi ni mtu mwenye midomo michafu, nami ninakaa kati ya watu wenye midono michafu; na macho yangu yamemwona Mfalme, Bwana wa Majeshi". Isa.6:5.

Mtu hawezi kujijua kuwa ana dhambi bila msaada wa Mungu. Kwa kuona Ukuu wa Mungu, mtu anatambua unyonge wake. Kwa kuona utukufu na Uzrui wa Mungu mtu anaona dhambi na makosa yake.

Baada ya Nabii kujitambua, Malaika wa Mungu alimtakasa kwa kaa la moto, Isa 6:6-7. Kwa kutakasa maovu ya zamani, pia kwa kutakaswa kutoka hali ya dhambi iliyopo ndani mwetu, unahitajika moto! Moto huu nitauongelea zaidi huko mbele, kwa sasa tujue wazi kuwa, kwa kupiga hatua yoyote kiroho, Mungu mwenyewe ndiye mhusika mkuu, na mtu kazi yake ni kumruhusu Mungu afanye kazi yake anavyoona yeye inafaaa.

Sasa mtu ameshajiona alivyo, na hapo mapambano ya kiroho yanaanza. Kadiri ya maumbile, mtu anapenda ajione mzuri na wa maana, na wengine pia wamwone hivyo. Hapa sasa inajitokeza kinyume. Ni sasa mtu anakaa chini mara ya kwanza na kukubali kuwa yeye si mzuri alivyotazamia, bali yeye anayo makosa na ni mdhambi. Ni vigumu sasa kukubali hali hii, kwa sababu hiyo yanaanza mapambano ndani ya mtu mwenyewe.

Tunaweza kusema hapa ndipo mwanzo wa safari ya kiroho. Ili safari hii iendelee mtu anahitaji kujizoeza katika fadhila ya UNYENYEKEVU na kuishi kile Bwana wetu Yesu Kristo alichosema : "Mtu yeyote akitaka kunifuata, na ajikane mwenyewe, ajitwike msalaba wake kila siku, anifuate". Lk.9:23. Kuchukua msalaba siyo kazi rahisi, kukubali hali ya ukosefu siyo rahisi. Watu hawa walioguswa hivi hugawanyika makundi mawili.

**Kundi la kwanza**
Ni wale ambao hawataki shida za njiani, wanajenga vibanda kando ya bahari, wanaendelea tu kuimba na kushangilia : "Praise God, Alleluia! … " Watazunguka-zunguka tu eneo la bahari wakisimulia namna Mungu alivyowavusha, furaha yao ni kumsifu Mungu. Lakini ukigusa undani wao ni kosa. Yote yaliyokuwa ndani yamefunikwa na masifu. Kwa vile hawaendelei mbele watarudi nyuma, na kuanguka katika makosa yafuatayo :

* Wanakuwa na majivuno ya kisiri-siri
* Kujiona watakatifu kuliko wenzao
* Hawafundishiki tena
* Kuwahukumu wengine ambao hawasali kama wao.

* Wanajishika na mambo matakatifu kama vile : misalaba, biblia, rozari, ibada za pekee na za mara kwa mara.
* Wanajiona kujua kuliko mtu mwingine hata kumrekebisha mwalimu.
* Wanamkwepa mwungamishi asije akajua kuwa ametenda dhambi ya aina hiyo, hivyo anaungama kwa mwingine. Akifuka kwa mwungamishi anaongea mambo mazuri mazuri tu.

Kinachowafanya watu hawa kufanya hivyo ni ukosefu wa UNYENYEKEVU. Amesahau kuwa Mtakatifu ni Mungu, nasi sote tuna midomo michafu. Asipokubali hali yake na kumwomba Mungu msaada, atabaki hapa hapa akijieneza mwenyewe na kuzunguka ufuoni mwa bahari akiimba masifu tu, na hapo ndipo mwisho wa safari yake ya kiroho.

**Kundi la pili**
Ni wale waliopigwa na hiyo nuru na kukubali hali yao ya udhaifu kwa unyenyekevu. Baada ya kujitambua na kujikubali, Malaika mwenye kaa la moto hujia na kumtakasa. Kundi la kwanza walipoona kaa la moto walikimbia kwa kuogopa maumivu ya kuchomwa. Hawa ni tofauti; wanatulia kama Nabii alivyotulia, wako tayari kukabili hali halisi, na hivyo wanakua katika fadhila. Baada ya kuona dhambi zao, mtazamo wao unakuwa tofauti na ule kundi la kwanza :
* Wanakubali kuwa wao ni wadhambi
* Wako tayari kudhalilishwa.
* Kutokana na Ukuu wa Mungu waliouona, hata wakisifiwa kwa lolote wanaona hawastahili.
* Wakiwaangalia wengine wanawaona wao kuwa bora zaidi.
* Wako tayari kujifunza kwa unyenyekevu hata kutoka kwa watu wadogo, mradi wapate kitu cha kuwasaidia kuendelea kukua katika kumjua Mungu.

Roho wa Mungu hufanya makao ndani ya watu wa namna hii.

Kuwa na mwelekeo huu wa unyenyekevu, ndiko kutakaswa kwenyewe kwa sababu kadiri ya maumbile yetu, mtu huelekea kujiinua na kuonekana bora. Kufanya kinyume chake kunasababisha maumivu

makali ya kiroho, lakini atakayevumulia mpaka mwisho ndiye atakayeokoka.

## MASOMO YA TAFAKARI

| | |
|---|---|
| Efe. 3:14-21 | Mpate kujua upendo wa Kristo upitao elimu zote |
| Gal. 5:1,13-14 | Ninyi ndugu mliitwa muwe watu huru. |
| Isa. 41:9-13 | Usiogope nitakusaidia |
| Isa. 49:1-16 | Wakati wa kufaa nilikujibu ombi lako |
| Kumb. 1:29-32 | Usiwe na hofu, umemwona Bwana Mungu wako |
| Hos. 11:1-12 | Israeli alipokuwa mtoto nilimpenda |
| Zab. 103 | Sifa za wema wa Mungu. |

*************************

# Siku ya 3
# Safari jangwani

Soma Kut. 15:22-17:7

**MAJARIBU YA KIROHO** (Late Purgative)

Tunaendelea na safari, wa kubaki kando ya bahari wamebaki sisi, tuendelee mbele. Tumeshaacha bahari mbali hatuoni tena. Tunalelekea nchi aliyotuahidi Mungu, mbele hatuoni kitu isipokuwa tu upepo wa hari jangwani unatupiga machoni. Waisraeli walikuwa na safari ngumu. Maji yaliwaishia njiani wakateseka sana kwa kiu. Chakula nacho kilikwisha, na bado wanakabiliwa na vita wakipigwa na watu wa huko jangwani. Kweli walikuwa na maisha magumu.

Hali ya ugumu wa namna hii ndiyo iwapatayo watu wa maisha ya kiroho walio tayari kuendelea mbele. Daima wanakumbuka kuwa : Mimi ni mdhambi, ni mdhaifu, lakini hata katika hali yangu hii isiyopendeza, Mungu ananipenda. Tena ananipenda katika hali yangu hii, kwa hiyo anapenda kunitakasa kabisa, kwa hiyo napokea kila kitu anachonipelekea.

Watu hawa wanatamani sana kupata mafundisho na semina mbalimbali, na wakipata wanatumia muda huo kwa shukrani. Nafasi ya semina ikipatikana lakini ikachukuliwa na mwingine, anakubali kwa moyo mweupe na kuona kuwa bado Mungu anamfikiria, na pengine huyo aliyechukua nafasi hiyo alihitaji zaidi.

Watu hawa wanaleta amani katika familia zao na katika jamii kwa ujumla. Hawana maneno mengi ya bure, zaidi ni watendaji. Kutokana na unyenyekevu wao, Mungu anawapenda sana na hivyo hawaachii. Uwepo wa Mungu kwao unaanza kuonekana katika kupitishwa kwenye moto makali wa kuwatakasa ili kuwasaidia kuendelea mbele kiroho. Moto huo waweza kujitokeza katika hali zifuatazo :

Wakisali hawapati jibu la sala zao

Waanona wengine wana vipaji vingi na vikubwa vya kiroho, lakini wao wakijiangalia hawaoni kipaji chochote.

Ugonjwa wa muda mrefu.

Ukosefu wa mahitaji ya lazima kama chakula, mavazi, nyumba, nauli ya kwenda semina.

Kudhaniwa au kusingiziwa mambo makubwa ya kuharibu jina.

Mungu anaonekana kuwa mbali.

Vishawishi vya kukosa imani na kuwa na mashaka na uwepo wa Mungu.

Majaribu ya wakati huu yanategemea mtu na mtu na kadiri Mungu alivyokusudia kumwinua. Kwa wengine itachukua muda mrefu, na wengine muda waweza kurefuka sana hata kufikia miaka. Hii ni hali ambayo ni ngumu sana, nayo huwapata wale wachache ambao wako tayari kumtanguliza Mungu mbele. Kwa kufanya hivyo inadai kufa, yaani kufia nafsi. Mtu anayaacha yale yote anyopenda ili afanye anayopenda Mungu. Kutokana na madai yake makubwa, ni hapa mtu anakata shauri : Nimfuate au nirudie maisha ya zamani ? Bwana Yesu alisema : "Mtu aliyetia mkono wake kulima, kisha akaangalia nyuma, hafai kwa ufalme wa Mungu". Lk.9:62.

Watu wanapopitia majaribu haya makali, wengi hushindwa na kurudi nyuma. Hata wale walioona miujiza alivyofanya Yesu walirudi na kumwacha, wanabaki tu wale kumi na wawili. Wengi waliojiita wafuasi wake, walipoona huo ugumu, waliondoka mmoja mmoja. Yesu akawauliza wale kumi na wawili : "Je, ninyi nanyi mwataka kuondoka ?". Basi Simoni Petro akamjibu, "Bwana! Twende kwa nani ? Wewe unayo maneno ya uzima wa milele" Yoh.6:67-68.

Tunapoendelea kuchunguza safari ya kiroho, tujikaze tuuone ukweli wote na madai yote ya kukua. Tunavyosikia katika Injili, watu wanaokusanyika kumsikiliza Yesu, mara nyingi ni maelfu ya watu, iweje

wabaki tu kumi na wawili ? Hata hawa kumi na wawili ni neema za Mungu zimewashikia hapo. Tukumbuke Yesu alivyosema : "Hakuna mtu awezaye kuja kwangu isipokuwa amejaliwa na Baba yangu" Yoh.6:65.

Sisi ni kazi ya mikono yake Mungu, na wokovu wetu watoka kwake, lakini mtu aweza kuukataa na kuupokea.
Wanaoupokea ndio wanatakaswa kwa majaribu mbali mbali. Ni wachache wanaoweza kustahimili hali hii ngumu ya kiroho, na hao ndio Mungu aliokusudia kuwafikisha mlimani Sinai ambapo Mungu atajitokeza kwao kuwafariji na kuwapa maagizo. Wakishika maagizo hayo, wataweza kuingizwa katika nchi ya Ahadi. Kwa vingine watafia vitani. Majaribu haya yanaleta maana ya maneno ya Mtume Petro aliposema : "ili kujaribiwa kwa imani yenu, ambayo ina thamani kuu kuliko dhahabu ipoteayo, ijapokuwa hiyo hujaribiwa kwa moto, kuonekane kuwa kwenye sifa na utukufu na heshima katika kufunuliwa kwake Yesu Kristo." 1 Pet.1:7.
Wote waliovumilia hayo, sasa wanakaribia kupiga hema chini ya mlima Sinai.

**MASOMO YA KUTAFAKARI**

| | |
|---|---|
| Zab.139 | Bwana umenichunguza na unanijua |
| Isa. 49:1-16 | Nimekuchora katika viganja vyangu. |
| Yer.18:1-12 | Mfinyanzi. |
| 1 Yoh. 4:10-19 | Mungu alitupenda kwanza |

| | |
|---|---|
| Mt. 6:24-34 | Ndege na mana ya jangwani. |
| Lk. 1:26-38 | Unyenyekevu wa Maria |
| Mk. 10:17-31 | Kijana tajiri |

***************************

# Siku ya 4
# Mlimani Sinai

Soma Kut. 19:1-31:18

**MUNGU ANATOA MWANGA : FURAHA YA UFUASI** (Illuminative)

Waisraeli walijitahidi kwa shida na taabu kuendelea na safari yao jangwani. Sasa wanafika mlimani Sinai. Wanapiga hema kadiri ya maagizo ya Mungu. Mahali hapa Mungu aliwatokea juu ya mlima, akaongea nao, akafunga agano nao na kuwapa maagizo mengi jinsi ya kuenenda ili waweze kufika salama nchi ya Ahadi.

Tukirudi katika safari yetu ya kiroho, Mungu anatoa pumziko la muda. Anawaruhusu watu wake wapige hema wapumzike kidogo. Katika hatua hii Mungu anajifunua

kwa watu wake. Watu wanafarijika kwa ajili ya mawasiliano hayo. Mungu anawaangazia, na mambo mengi yanakuwa wazi kwao. Wanafurahi tena wito wao.

**MASUKUMO WAO WA NDANI**

Katika safari ya kiroho ni wachache sana wanaofaulu katika mlima Sinai, kwa sababu kwa kila hatua wapo wanaorudi nyuma, na wengine kufia vitani. Hawa wamejaliwa kupita salama hatari zote za kiroho hadi hapa Sinai. Hamu yao kubwa sana ni kuwa na Mungu, kuongea habari za Mungu kwa utulivu na kusikiliza habari za Mungu. Pamoja na mazingira yote yanayozunguka, mawazo yote ni kwa Mungu wakiwaza wampendeze namna gani. Wako tayari kuingia hasara kwa ajili ya Mungu. Daima wawapo kazini wanamfikiria Mungu. Wako tayari kutumia nguvu zao, pesa zao, muda wao ili Mungu atukuze. Pamoja na kazi zinazowakabili kijamii, watajitahadi kujipatia muwa wa kukaa na kutulia mbele ya Mungu katika sala.

Ni watu wenye ari kubwa sana ya kutangaza Neno la Mungu kwa sababu wameangaziwa kwa namna ya pekee katika hatua hii. Hawawezi kutulia. Mtume Paulo alipokuwa katika hatua hii alisema : "Ole wangu nisipoihubiri Injili", 1 Kor.9:16.

Watu hawa wanatamani watu wengi iwezekanavyo wafikiwe na hii Habari Njema, kwani hakuna kitu kizuri zaidi ya kumjua Kristo. Mashahidi wengi yaani watu wengi waliokubali kufa kwa ajili ya Kristo wanatoka katika hatua hii. Watu hawa wana uhakika na wanachokiamini, wana uhakika na wanachokisema, wana uhakika na wanachokihubiri. Wana hamu kubwa ikiwezekana watu wote waonje utamu na uzuri wa kumjua na kumpendeza Mungu. Watokapo katika kazi ngumu na pengine ya hatari ya kitume, furaha yao ni kutulia mbele ya Bwana katika sala na kujazwa tena nguvu mpya.

Mungu anawaacha hapa kwa muda wakifarijiwa. Hawana wasiwasi, na wanawatakia wote mema. Hawana uadui na yeyote kwani walikwisha wasamehe wote. Kwa kawaida muda huu wa faraja unatofautiana mtu na mtu kadiri ya utayari wake kwa kupokea mambo asiyoyajua. Pamoja na yote hayo, bado hawajafika. Kila hatua yapo majaribu yake. Majaribu ya hatua hii ni makali kuliko yote yaliyotangulia. Moto huu unapaswa kuwa mkali hivyo uweze kuunguza kila kitu ambacho kilikuwa kigumu kuungua kwa njia ya moto uliotangulia.

**MATESO NA MAUMIVU YAO**

Wateule hawa bado, siyo wakamilifu, wanaendelea na mapambano bado. Mapanbano yao ni makali sana. Katika hatua zilizopita waliingizwa katika moto na katika giza ili kutakaswa. Kumbe kutokana na hali ya mtu na yale aliyozoea zamani au yaliyomwumiza, kuna mengine

yaliyokuwa na mizizi ya ndani hivyo kwamba, mtoto uliotangulia haukuweza kuteketeza kila kitu.
Sasa katika hatua hii ni lazima kila kitu kisicho Mungu ndani ya watu hawa kiangamizwe! Hii ndiyo hatua ya mwisho ya kusafisha, na moto wake unalazimika kuwa mkubwa sana na mkali sana. Mara nyingi hali hii moto wake waweza kujitokeza katika hali zifuatazo :

Kutopata kitulizo chochote katika sala.
Ukavu wa sala unaodumu muda mrefu hata kufikia miaka.
Kutoona faida karibu katika kila kitu.
Kutoona maana au thamani ya maisha ninayoishi sasa (Utawa, Upadre, Ndoa - uchunguzi mbaya wa mwenzi wa ndoa …. )
Mungu kuonekana kuwa mbali.
Kila kitu kinakuwa cheusi cheusi na bila matumaini.
Mwelekeo mkubwa wa mkato wa tamaa.
Kutamani kufa na kuwaonea wivu waliokwisha kufa.
Kuwa na mashaka na uzima wa milele.

Hali hii ni ngumu kuliko zote walizokwishapitia. Ni ngumu kuliko mtu anavyoweza kuandika juu yake. Pengine ningeweka hali hii katika mfano nitasema :
Ni kama mtu aliyepanda ngazi refu sana, akafaulu kukaribia mwisho wa ngazi, lakini akashindwa kukanyaga ile ya mwisho kwa sababu hana pa kujishika. Akakazana kujiinua kwa kutumia kifua, sasa anajaribu kukanyaga anashindwa bado, anajaribu kurudi nyuma akanyage ile aliyoicha sasa hivi, anashindwa. Anabaki akining'inia na wakati huo ngazi inaanza kucheza-cheza, ikiyumba-yumba na kutaka kuanguka. Kwenda mbele hawezi, kurudi nyuma hawezi, kujiachia aanguke ni mbali mno atapasuka vipande vipande.

Maumivu ya watu wa hatua hii ni makali na ya kutisha kuliko hata mfano huu unavyoeleza kwani ni maumivu ya kiroho yasiyo na lugha ya kuelezea. Hakuna

mwanadamu awezaye kupita salama peke yake bila msaada wa Mungu. Mtu aliye katika hali hii ya kuning'inia, yambidi kunyenyekea sana na kupiga ukelele wa kuomba msaada. Ndio wakati wa kuomba watu wakuombee, kumwomba mama Bikira Maria akuombee, ndio wakati wa kusali rozari mfululizo. Ni wakati wa kuomba msaada kokote upatikanapo. Ni kweli Mungu anao uwezo wa kusaidia bila kupitia kote huko, lakini kumbuka kuwa ni majaribu ya utakaso na kwa njia hiyo atafurahi tukinyeneyekea. Pia tukumbuke mtu wa hatua hii anapambana na mkato wa tamaa na tena haonji tena uwepo wa Mungu, kumbe asipoomba aombewe, aweza kukata tamaa.

Maumivu haya yaweza hata kufikia miaka. Hapa inategemea mtu na mtu. Jaribio likipita, lingine linafuata mara. Jaribio linaita jaribio. Wakati maalumu ukifika, wakati alioona Mungu inatosha kwa sasa, anatoa amani na pumziko. Furaha na utulivu vinarudi tena, ila kwa sasa inakuwa furaha kubwa zaidi na ya ndani sana kuliko ya awali kwa sababu aliyoyapitia yamemsogeza karibu na Mungu zaidi. Iwapo kuna bado kitu kilichobakia, atasuburi mtu akusanye tena nguvu na baada ya muda tena anarudishwa katika mapambano. Itaendelea hivyo hadi atakapoona hakuna doa lililobaki.

**MASOMO YA TAFAKARI :**

| | |
|---|---|
| Zab. 51 | Unihurumie ee Mungu. |
| 2 Sam. 11:1-25 | Daudi na Bethsheba. |
| 2 Kor. 12:1-10 | Ninapokuwa dhaifu ndipo ninapokuwa na nguvu. |
| Ebr. 2:14-18 | Yesu alijaribiwa kama sisi. |
| 1 Yoh. 1:5-10 | Mungu atatusamehe dhambi |
| Lk. 19:1-10 | Zakayo |
| Lk. 18:9-14 | Mfarisayo na mtoza ushuru. |
| Lk. 22:54-62 | Petro analia. |

*********************************

# Siku ya 5
# Ndama ya dhahabu

Soma Kut.32:1-6

**MAJARIBU KATIKA HATUA YA UANGAZO** (Illuminative)

Waisraeli wapo bado mlimani Sinai. Mahali hapa ni pa maana sana katika historia yao kwani hapa Mungu
alikutana nao na kuwaangazia kwa kuwapa maagizo na amri zake. Hapa wanamtambua Mungu zaidi, kwa kupitia Musa mtumishi wa Mungu. Pamoja na kuangaziwa, bado nafasi za kuanguka zipo. Musa alipokawia mlimani, Waisraeli walipata nafasi ya kuanguka kwa kuitengeneza sanamu ya ndama wa dhahabu na kuiabudu.

Hatua waliyoifikia Waisraeli, ni hatua ya kawaida kabisa kwa safari ya kiroho ya mtu binafsi. Baada ya mtu kupiga hatua mbele kiroho, aweza bado kuanguka, na yule Mwovu mshawishi anajua mbinu za kutumia ili awaangushe watu hawa ambao walishasonga mbele sana kiroho. Wakati Mungu anapoendelea kumtakasa mtu wake na yule Mwovu yupo karibu. Kwanza tuone majaribu ya wakati huu.

**GIZA NENE NA UKAME WA ROHO**

Mungu anamwingiza mtu huyu katika giza kuu ambako kila kitu kinavurugika.

Kile alichofurahia zamani haoni uzuri wake tena.
Kazi aliyoizoea na kuipenda, haoni faida yake tena.
Hujionea huruma kwa kupoteza muda kwani haoni alichofanya mpaka sasa.
Hata sala zake anaona hazifiki kwa Mungu tena.
Alishakuwa na ari ya kutangaza Habari Njema na kupenda kusali; sasa haoni maana yake hata kidogo. Faraja kwa mtu huyu haipo kabisa wala kutoka ndani mwake wala kutoka nje yake, misaada yote imeondoka !

Kama alipata msaada kutoka kitabu fulani, au kitachukuliwa au hakielewi tena au kitachomeka. Kama ni mtu alimfariji, au atahama, au atamwelewa kinyume, au hatakuwa na muda naye au atakufa ! Kutatokea kitu kilete kutoelewana na wazazi, ndugu, marafiki, kazini, na wale wote waliomwona wa maana watakwazika na kumgeuka. Marafiki zake wanageuka kuwa maadui. Wanamsengenya kila mahali. Watu wote wa karibu wanapoteza imani naye, vikundi kwa vikundi wanamsema, akijaribu kujichanganya na kundi fulani, akifika wanakaa kimya, hapa na pale anasikia minong'ono juu yake, hana pa kukimbilia. Mzabuiri alipofikia hatua hii alilia : "Ee Mungu uniokoe, maana maji yamefika mpaka nafsini mwangu…. Wanaonichukia

bure ni wengi kuliko nywele za kichwa changu. … Waketio langoni hunisema, na nyimbo za walevi hunidhihaki … ! Zab. 69:1-21.

Mtu huyu anajisikia mpweke hata katika jumuiya kubwa. Matatizo yanamzunguka kila upande, haeleweki wala hajielewi !

Moto huu ni mkali na madhumuni yake ni kuteketeza kila kitu, yote ya kibinadamu yanateketezwa ili ibaki ya Mungu tu. Yote haya ni ya lazima ili kuweza kumtakasa mtu na mwelekeo wake wote wa kibinadamu. Mtu anateseka si kwa sababu ya dhambi zake au za mtu mwingine bali ni kwa sababu ya ubinadamu wake. Mwanadamu anatolewa katika hali duni ya kibinadamu na kuingizwa katika hali ya Kimungu. Dhahabu inapochomwa imekosa nini ? Lengo lake ni kutakaswa (1 Pet. 1:6-9). Jinsi dhahabu inavyotakaswa, ndivyo na roho inavyotakaswa.

Kwa mantiki hiyo, "Toharani ni lazima kosa usikose !" Kila mtu ni lazima kutakaswa ili aweze kufaa kuwekwa katika hali ya juu pamoja na Mungu au ndani ya Mungu. Kwa wale waliofikia hatua hii na kupita salamu majaribu yote, toharani yao watakuwa wameimalizia hapa hapa

duniani. Wale ambao hawakufikia hatua hii, toharani
inawasubiri baada ya kufa, yaani kabla ya kumwona Mungu, kwanza watapata mateso ya kuwatakasa. Tukijua hivyo tujikaze tupokee kila umivu kwa uvumilivu !

**KASORO NA MADHAIFU YAO**

Kama Waisraeli walivyotengeneza ndama wa dhahabu na kumwabudu, watu wa hatua hii nao wapo katika hatari ya kuanguka katika madhaifu yafuatayo :

Anapata kishawishi cha kujiona mtakatifu.
Ana majivuno ya siri siri sana, mwenyewe aweza pia asijue
Aweza kuadhalilisha wengine kwa kuwaona wadhambi.
Anaweza kuona kwa urahisi makosa madogo madogo hasa ya viongozi wa dini.
Anaweza kulalamika kwa ajili ya makosa ya wengine na kazi zao.
Ataweza kupenda mambo matakatifu, na kuyaweka mahali pa heshima kiasi cha kumsahau Mungu.
Anaisifu sana kazi yake.

Ili kuponywa na hali hii, moto wa utakaso utapita tena. Wenye kujirudi wanarudi, wengine wanashupaa. Wanakuwa na shingo ngumu. Hawa ni wagumu sana kuwasaidia kwa sababu wanajiona wanajua, wanajiona watakatifu. Waweza kuongeza ukaidi kiasi cha kufikia kuwa wazushi na hata kujitenga na Kanisa.

Yapo mengi ya kuongea katika hatua hii, lakini napenda kukatiza hapa nikisema kuwa kitakachorahisisha safari hii ya kiroho ni kuwa MNYENYEKEVU, kwa vingine mtu

aweza kutoka nje kabisa au kwenda mbele nyuma, mbele nyuma, bila kuendelea. Tumshukuru Mungu aliye kiongozi mkuu wa safari hii.

**MASOMO YA TAFAKARI :**

| | |
|---|---|
| Hos. 2:16, 21-25 | Nitamhurumia asiyehurumiwa. |
| Lk. 9:57-62 | Wanaostahili kuwa wafuasi. |
| Lk. 15:11-31 | Mwana mpotevu. |
| Mt. 9:9-13 | Mathayo anaitwa. |
| Yoh. 21:15-19 | Petro mwana wa Yona wanipenda ? |
| Mdo. 22:6-16 | Ndugu Saulo, ona tena. |
| Mdo. 10:34-48 | Hotuba ya Petro. |

********************************

# Siku ya 6
# Nchi ya maziwa na sala

Soma Yos. 5:6

**MJI WA MWANGA NA UTOSHELEZO**

Soma Ufu. 21:1-27.

**UANA WA MUNGU** (Unitive)

Waisraeli wale waliopita salamu jangwani wanaingia nchi ya Ahadi, nchi itakayokuwa yao, nchi ambayo ni ishara ya ile ya mbinguni. Ni nchi iliyojaa maziwa na asali, maana yake ni nchi iliyo na utajiri mwingi, nao Waisraeli ndio warithi wa nchi hiyo. Mji huo ni kama alivyojaribu kuandika Mtakatifu Yohane katika Ufu. 21.

Tukirudi katika safari yetu ya kiroho, kila mmoja anatamani sana kuingia katika mji huyo, lakini tumeona masharti magumu ya kuingia huu mji au hii nchi ya Ahadi. Pia tukumbuke mtu akitaka kitu cha thamani ni lazima akitokee jasho.
Tangu mwanzo wa safari hii tuliona kuwa moyo wa mtu hautatulia mpaka uunganike na Muumba wake. Wote waliomtafuta wakijua wanachofanya, wakawa tayari kuikabili kila hali ndio hao Mtume Yohane anaosema juu yao : "Wote waliompokea aliwapa uwezo wa kufanyika watoto wa Mungu, ndio wale walioaminio jina lake." Yoh. 1:12.

Kwa sababu hii tuliumbwa ili tupewe hadhi ya kuwa wana wa Mungu. Anayeshindwa kufika hapa amepoteza sana, ameingia hasara ya maisha laiti mtu huyo asingalizaliwa kwa sababu hakufikia lengo la kuzaliwa kwake. Mtu aliyefaulu kufikia hatua hii akiwa duniani au hata baada ya kufa, huunganishwa kabisa na Mungu. Muungano huu ni wa ndani sana. Ni kama mito inavyotiririkia baharini; maji yafikapo baharini huchanganyika na mengine kiasi ambacho hutajua tone lipi ni la mto gani ? Yote yanajulikana kama bahari. Hata roho za wateule waliofaulu katika mapigano na hatimaye kuunganishwa na Mungu kabisa. Ninaweza kusema : Wote wapo lakini ni Mungu tanamwona kwa sababu wote wamegeuzwa na kupewa hali ya Kimungu, hivyo yote yatakuwa ya Kimungu. Kama kungekuwa na rangi, ni ya Kimungu, kama kungekuwa na harufu, ni ya Kimungu. Yote yanakuwa ya Kimungu.

Safari hii ni refu na ngumu. Wanaoweza kupitaa hatua zote za utakaso hapa duniani ni wachache sana. Wengi tunaowaona kuwa ni watu wenye bidii sana kwa mambo ya Mungu hata tukafikiri ni watakatifu, wengi wao huishia mlimani Sinai. Ni wachache sana wanaoweza

kustahimili hadi hatua ya mwisho. Ukichunguza watu wote wanaoishi duniani sasa, pengine utakaowapata waliofikia hatua ya mwisho watahesabika katika makumi !

Tumshukuru Mungu aliyetuonea huruma akaweka toharani hali ya kutakasa tunapobakiwa na madoa. Tulioko sasa safarini tujielimishe kujizoeza unyeneyekevu, na huu utatuwezesha kupiga mbio za kiroho hadi tutakapoingia ule mji unaodumu, mji wa Mungu wa milele, tutakaposifu bila mwisho.

**TAFAKARI NA MJADALA :**

| | |
|---|---|
| Lk. 9:28-37 | Yesu ageuka sura. |
| Yoh. 17:20-26 | Yesu anawaombea waamini wote. |
| Yoh. 20:11-18 | Mama, unalia nini ? |
| Yoh. 21:1-24 | Yesu anawatokea wanafunzi kando ya ziwa Tiberia. |
| Lk. 24:13-35 | Emmaüs. |
| 1 Yoh. 2:24-27 | Ujumbe mliosikia tangu mwanzo na ukae mioyoni mwenu. |
| 1 Pet. 1:3-35 | Kristo Mfufuka anatupatia tumaini jipya. |

**Baada ya kusikia haya yote :**

Nifanye nini ?
Tufanye nini ?

************************